**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

# TAKUKURU KAGERA YAJIPANGA KUFANYA TAMASHA LA MTOTO WA BUKOBA KUDHIBITI RUSHWA

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTENDAJI WA TAKUKURU MKOA WA KAGERA KUANZIA JULAI 2018 HADI MARCH 2019 ILIYOTOLEWA KWA WAANDISHI WA HABARI

---

**KAGERA JUNI 7, 2019**

## 1.0 Utangulizi

Ndugu wanahabari, ni imani yangu kuwa kila mmoja wetu anafahamu kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria za nchi na maandiko matakatifu hasa kutoka katika Vitabu vitakatifu vya **BIBLIA** na **QURAN** zinakataza mtu yeyote kujihusisha na vitendo dhidi ya rushwa. Kwa hiyo, mtu yeyote kujihusisha na vitendo dhidi ya rushwa ni kukiuka Sheria za nchi na kwenda kinyume na Maandiko matakatifu ya Mwenyezi Mungu. Ndio maana Sera ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kutovumilia vitendo vya rushwa (**zero tolerance to**

**corruption**) na kwa msingi huo kila mtanzania hapaswi kabisa kujihusisha na vitendo vya rushwa. Watanzania kwa ujumla wetu tunapaswa kuhakikisha kwamba tunazuia na kupambana na **rushwa** hapa nchini.

Taarifa hii ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inaonyesha utendaji wa TAKUKURU kuanzia Julai 2018 hadi Machi 2019, na sehemu ya pili inaonyesha vipaumbele vyetu katika utendaji kazi kwa kipindi cha Machi 2019 mpaka June 2019.

**2.0 Utendaji Kazi Kuanzia Julai 2018 hadi** Machi **2019**

Taarifa hii imezingatia utekelezaji wa malengo katika maeneo ya Uchunguzi, Uelimishaji umma na Udhibiti wa vitendo vya rushwa.

### 2.1 Uchunguzi

Takwimu zifuatazo zinaonyesha utendaji kazi wetu katika uchunguzi kwa kipindi cha kuanzia 1.7.2018 hadi tarehe 30.03.2019. Pia ni vyema ikafahamika kuwa katika Chunguzi zinazofanyika tunashirikiana sana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na hivyo katika ufunguaji na uendeshaji wa mashauri tunashirikiana sana na ofisi hiyo.

| **Na.** | **Maelezo** | **Jul 2018 –March 2019** |
|---|---|---|
| 1 | Taarifa zilizopokelewa | 440 |
| 2 | Majalada yaliyofunguliwa (RB) | 100 |
| 3 | Majalada yaliyokamilika | 50 |
| 4 | Majalada yanayoendelea na Uchunguzi | 230 |
| 5 | Kesi zilizofunguliwa Mahakamani | 41 |
| 6 | Kesi zinazoendelea Mahakamani | 45 |
| 7 | Kesi zilizoamuliwa Mahakamani | 25 |
| 8 | Kesi zilizoshinda Mahakamani | 15 |

| | | |
|---|---|---|
| 9 | Kesi zilizoshindwa Mahakamani | 10 |

Malalaiko ambayo yanapokelewa katika wilaya za Mkoa wa Kagera yanatofautiana. Kila wilaya imekuwa ilipokea aina tofauti ya malalamiko ingawa kuna baadhi ya malalamiko yanafanana kama ifuatavyo;-

Katika wilaya za Bukoba. Muleba na Karagwe malalamiko mengi yanatokana na migogoro katika Ardhi hususan kuingiliana katika mipaka, kughushi Wosia, kughushi nyaraka za mauziano ya viwanja na mashamba

Sanjari na aina hiyo ya malalamiko pia kumekuwepo na malalamiko mengi katika uendeshaji wa Mabaraza ya Ardhi na mabaraza ya Kata ambapo baadhi ya wajumbe wa mabaraza hayo wamekuwa hawazingatii taratibu za uendeshaji wa mabaraza hayo na hii inasababishwa na wajumbe wengi kutopatiwa mafuzo ya uendeshaji na wengine kutokuwa waadilifu na tamaa hali iliyopelekea wengine kujianzishia gharama za tozo tofauti na zilizoidhinishwa na Bylaws.

Pia katika wilaya za Bukoba, Misenyi, Muleba na Karagwe kumekuwepo na matatizo yanayohusiana na baadhi ya watu kujifanya maafisa wa TAKUKURU, Usalama wa Taifa na POLISI hali hii imezua hofu miongoni mwa wananchi. Pamoja na Serikali kutoa tahadhari nyingi kwa kushirikiana na mitandao ya simu lakini bado kuna malalamiko katika wilaya nilizozitaja.

Katika wilaya za Bukoba na Karagwe kumekuwepo malalamiko ya ubadhirifu wa fedha za miradi ya maendeleo na fedha za vyama vya ushirika. Hali hii inasababishwa sana na baadhi ya watumishi ambao wamekuwa sio waadilifu na wengine wana tamaa.

Biharamulo penyewe pamekuwepo na malalamiko katika Migodi ya madini ya dhahabu hasa katika utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya ununuzi wa vilainishi na kemikali muhimu zinazotumika katika uchenjuaji wa madini.  Hii imetokana na baadhi ya watendaji na wafanyabiashara kutokuwa waadilifu na wenye tamaa

Kaitka wilaya za Ngara, Biharamulo, Kyerwa na Misenyi kumekuwepo malalamiko katika fedha za Mfuko wa Pembejeo .

Wilaya ya Missenyi pia yamekuwepo malalamiko ya rushwa katika utoaji wa vibali vya muda vya kusafiria hali iliyopekea kuanzishwa kwa kunguzi ili kuweza kuthibitisha tuhuma hizo.

Katika Wilaya zote yamekuwa yakipokelewa malalamiko yanayohusiana na jeshi la Polisi matatizo ya kuomba rushwa , kubambikwa kesi na pia malalamiko yanayuhusiana na makusanyo ya ndani  mfano katika minada na stand . Vilevile malalamiko katika  utoaji wa vibali vya ujenzi toka katika halmashauri za wilaya na Manispaa.

## 2.2 Uelimishaji Umma

Katika kuhakikisha elimu ya mapambano dhidi ya rushwa inawafikia watu wengi hapa mkoani Kagera, TAKUKURU imekuwa ikitoa elimu kwa makundi mbali mbali kwa kuwahamasisha wananchi watambue madhara ya rushwa na namna ya kuzuia na kupambana na rushwa.

Takwimu zifuatazo zinaonyesha utendaji kazi wetu katika uelimishaji umma kwa kipindi cha kuanzia 1.7.2018 hadi tarehe 31.03.2019.

| NA | **MCHANGANUO** | **IDADI** | **IDADI**<br><br>YA WANACHAMA |
|---|---|---|---|
| 1 | Uimarishaji wa Klabu za Wanafunzi Wapinga Rushwa Mashuleni/Vyuoni | **194** | **3411** |
| 2 | Semina zilizofanyika kuelezea Madhara ya Rushwa | 144 | **3167** |
| 3 | Mikutano ya Hadhara Iliyofanyika Kuelezea Madhara ya Rushwa | **201** | **1867** |
| 4 | Kushiriki maonesho | **16** | **312** |
| 5 | Uelimishaji kupitia vyombo vya habari Raio na Television | **7** | **wengi** |

Mbinu hizi za ueimishaji zimetumika katika wilaya zote  za Mkoa wa Kagera na zimetumika katika kuwaelimisha wananchi katika maeneo mbalimbali . Kwa mfano wakati wa Sherehe za Sabasaba na nanenane  katika maeneo yote TAKUKURU tulikuwa na mabanda ya Uelimishaji na tulishiriki katika kuelimisha Umma  kwa kufanya mahojiano na wananchi , kugawa vipeperushi na kujibu maswali toka kwa wananchi.  Katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Sheria tulikuwa na Banda la uelimishaji na katika mbio za Mwenge pia tulishiriki kwa kuelimisha umma.

Waandishi wa Habari pia shahidi wetu wa namna tulivyoshirikiana nanyi katika kutoa elimu ya rushwa kupitia vipindi vya Radio. Radio Kasimbate, Radio Fadeco, Radio Kwizera na Radio Shinazi pamoja na Radio Vision tumweshiriki katika kurusha vipindi.
Katika wilaya ya Muleba tulifanya Uelimishaji kwa kutumia Gari la matangazo pamoja na kuonyesha -Filamu ya BAHASHA yenye maudhui ya elimu dhidi ya rushwa.

**2.3 Utafiti na Udhibiti wa Rushwa**

Mojawapo ya majukumu ya TAKUKURU ni kushauri namna bora ya kupambana na rushwa na namna ya kutambua mianya ya rushwa na kuiondoa. Takwimu zifuatazo zinaonyesha utendaji kazi wetu katika udhibiti wa vitendo va rushwa kwa kipindi cha kuanzia 1.7.2018 hadi tarehe 31.03.2019.

| NA. | MCHANGANUO | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | Idadi ya maeneo yaliyofanyiwa utafiti | 15 |
| 2. | Mikutano iliyofanyika kujadili matokeo ya utafiti | 7 |
| 3 | Miradi ya maendeleo iliyofuatiliwa na kukaguliwa | 23 |
| 4 | Thamani ya Miradi iliyofuatiliwa na kukaguliwa | **7,790,500,800/=** |

Uchambuzi wa mifumo uliofanyika, ulifanyika katika maeneo yafuatayo kwa kuwa maeneo haya yalikuwa yanalalamikiwa na vitendo dhidi ya rushwa;-

Bukoba, katika utendaji wa Jeshi la Polisi hasa katika Vituo; Utoaji wa vibali vya ujenzi Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba

Missenyi,na Ngara ulifanyika uchambuzi wa mfumo katika kubaini mianya ya rushwa iliyopo katika utoaji wa vibali vya muda vya kusafiria

Kyerwa, uchambuzi wa mfumo ulifanyika katika eneo la ukusanyaji wa mapato ya hususan mapato yatokanayo na ushuru wa mazao na ukusanyaji wa ushuru katika maeneo mengine.

Karagwe, tumefanya uchambuzi katika Baraza la Ardhi na Nyumba, Mahama na katika usambazaji wa Umeme wa REA.

Katika wilaya za Biharamulo, Karagwe na Muleba chambuzi za mfumo zilifanyika katika idara ya Afya tulitazama mianya ya rushwa katika utoaji wa huduma za Afya HASA afya ya mama na mtoto na wazee; Pia tuliangalia mianya ya rushwa katika jeshi la Polisi

**3.1 Vipaumbele kwa kipindi cha Machi 2019 mpaka Juni 2019**

Pamoja na utekezaji wa majukumu yetu ya kawaida pia tumejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

I. Kuongeza kasi ya uchunguzi katika tuhuma kwenye maeneo ya vyama vya ushirika, miradi ya maendeleo, ubadhilifu katika usambazaji wa pembejeo za kilimo na katika makusanyo ya fedha za ndani za Halmashari
II. Kuongeza kasi ya uelimishaji umma kwa kutumia njia mbalimbali mfano nyimbo, ngoma, mashairi na maigizo Filamu ya BAHASHA kupitia TV BUKOBA ( Tuko katika mazungumzo ili tuweze kupatiwa muda wa kurusha filamu hiyo ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha waandishi wa Habari ili waweze kushiriki vyema katika kuelimisha umma na mapambano dhidi ya ryushwa.,. Hivi karibuni tunatarajia kufanya tamasha la **MTOTO WA BUKOBA** lenye lengo la kukemea vitendo dhidi ya Rushwa tamasha hili litaitwa" BUKOBA TITUKWENDA EKYEMENYO"

III. Kuongeza kasi katika kufanya chambuzi za mifumo hasa katika maeneo yanayolalamikiwa zaidi hasa maeneo ya utoaji wa huduma kwa wananchi na katika miradi ya maendeleo
IV. Kufuatilia miendendo ya uchaguzi wa serikali za mitaa kabla ,wakati na baada ya uchaguzi.

**5.0 Hitimisho**

Tumalizie kwa kusema wazi kuwa uadilifu na nidhamu ni vitu vya msingi sana katika maisha ya binadamu. Kwa hiyo basi, watanzania kwa ujumla wetu tutafanikiwa kuzuia na kupambana na rushwa iwapo sisi sote tutakuwa **WAADILIFU NA** WENYE **NIDHAMU ya kazi** na

**NIDHAMU ya dhamana** tuliyopewa katika kutekeleza majukumu yetu yawe ya kifamilia au ya kijamii.

**Ninatoa rai** kwa watumishi wa umma na watanzania kwa ujumla kwamba wajiepushe na vitendo vya rushwa vinginevyo watalipia matendo yao hayo kwa uchungu mkubwa na kwa majonzi makubwa pale watakapofungwa jela.

**Pia ninatoa wito** kwa watanzania wote hasa wanaoishi mkoani Kagera kukataa kuomba, kupokea au kutoa rushwa na washirikiane na TAKUKURU ili kuwabaini wala rushwa na mafisadi wanaotumia vibaya madaraka yao na mali za umma ili wafikishwe mahakamani wakapate adhabu wanayostahili. Bora kila mmoja wetu akafahamu kuwa kujihusisha na vitendo dhidi ya rushwa ni kula kaa la moto kwani huwezi kulimeza lazima uungue

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

Imetolewa na:

JOHN K.E JOSEPH

**MKUU WA TAKUKURU MKOA**